# Gazeti la kimataifa
## Waabuduo Damu ya Kristo

... Kwa Neno Lako...

Lima, Peru
5-28 Luglio 2017

Mwaka XXI – N. 8 – Juni 2018



Waabuduo Damu ya Kristo - Uongozi Mkuu - Via Maria De Mattias,10 - 00183, Rome
www.adoratrici-asc.org
redazioneasc@adoratrici-asc.org


## Mhutasari


*Mhariri*
Wenye heri wa mlango unaofuata 1

*Nafasi kwa uongozi mkuu*
Maadhimisho ya siku ya tamaduni: mwaliko kuelekea mabadiliko 3

*Toka Ulimwengu ASC*
Huduma kwa mpendwa jirani 5
Mang'amuzi mazuri pamoja na wanandoa 7
Mpango mzuri sana wa Bara la Asia kwa Waabuduo wetu wa nadhiri za muda huko Philippine 9
Ziara ya mwisho huko Philippine 10
Maadhimisho ya watu 11
Siku ya ASC wa region ya Zagabria 12

*Nafasi kwa JPIC – VIVAT*
Jana, Leo, Kesho 13

*Ndani ya shirika ASC*
Kalenda ya Uongozi Mkuu 14
Heri na pongezi 14
Mikutano ya Regions na ya Foundation 14
Waliorudi nyumbani kwa Baba 14


Mhariri

# WENYE HERI WA MLANGO UNAOFUATA



Utakatifu ni zawadi

Kwa wengi ni zawadi ya gharama kubwa, lakini kwa uhalisia ni zawadi kubwa na siyotarajiwa ambayo hupita kwa mapendekezo ya "kutoizika", bali kuifunua. Papa Francis katika Mawaidha ya Kitume ya mwisho (Gaudete et Exultate/Furahini na Shangilieni) anatuonesha kwa njia ya Heri, chaguzi za utekelezaji wa utakatifu, ambazo hupitia chaguo la upendeleo kwa maskini ili kuondokana na aina zote za utengano, ubinafsi na kutojali.

Tunaishi wakati wa utandawazi wa kutojali na

wa wenye heri katika jamii wanaoitwa kupinga wale wanaonyonya wadhaifu, kuangalia hali halisi na kujaribu kuokoa watu wanaokufa kwa njaa na kiu, kutosahau wasio na makazi, wanaokosa elimu na kurejesha tena heshima na kazi, kuthamini kile ambacho mtu anacho na hakitumiwi, kwa sababu utakatifu sio jambo la kuwazika bali la kweli.

Wenye heri hawalipi fedha kwa chaguzi zao, bali kwa hundi za ufadhili, hufungua mioyo yao kwa kila mtu na kutopoteza muda katika mambo ya kila siku yasiyo na faida, ili kutambua Injili ya furaha, huvunja mantiki ya heshima ambayo mara nyingi huishia kutoa mashariti kwenye mapendekezo ambayo huondolewa kabla ya kuzaa matunda.

Maria De Mattias ni mtakatifu kwa sababu alizifanya Heri kuwa shamba lake la vitendo. Uchaguzi wake umekuwa uamuzi wa shamba, kwa kuwa alitoa nafasi za ukuaji wa mwanadamu mzima, akienda kinyume na utamaduni na desturi za wakati na kuchagua upande wa wanawake waliokandamizwa na jamii ya karne ya kumi na tisa.

Ni nani anajua angesema nini leo, wapi angependa masista wake wawepo.

Ni nani anayejua mipango ipi angeweza kuifanya mbele ya wanawake, kwenye janga lililokomaa la utoaji mimba au ukosefu wa elimu ya maadili ya kiinjili.

Hakika angeweza kusema kuvaa mavazi ya wanawake wa mapinduzi ya Injili kama ya Maria wa Nazareti, ya Magdalena aliyeongoka na ya mwanamke yule wa ajabu wa Samaria ambaye alitoka katika kuolewa na wanaume wengi hadi kuwa mmisionari.

Ni zamu yetu pia, kama Kanisa la milenia ya tatu, kama watawa wa "ulimwengu huu uliozeeka", kuupyaisha kwa chaguzi za kinabii na huruma.

Tunaitwa kuimarisha miundo yetu, kuunda njia za imani kwa ajili ya jumuiya zetu, kupyaisha tena kazi zetu na juu ya yote kuanza kuunga maneno ya utakatifu ambayo hayajibu tu kwa uwezekano, bali kwa utayari kamili kuelekea upyaisho.

**Sr Mimma Scalera, ASC**



# MAADHIMISHO YA SIKU YA TAMADUNI: MWALIKO KUELEKEA MABADILIKO

Uzoefu wa mwingiliano wa tamaduni sio tena kitu ambacho ("ni cha hiari kujenga" lakini leo umekuwa ni kitu cha lazima. Kwa bahati mbaya watu wengi wameandaliwa kidogo kupokea hali tofauti, kuwaelewa watu wa tamaduni zingine zilizotofauti na kupokea mwenendo wao kadiri ya desturi inayoendana na utamaduni mpya.



Kwa kweli wengi wanajiuliza kuhusu kwa nini lazima iwe wao wapokee. Kwa mtazamo wao wengine wanapaswa kupokea desturi zao au, angalau, pande zote mbili zinapaswa kutafuta namna ya kufikia makubaliano. Huu mtindo wa kufikiri hautupeleki popote. Ni watu wachache waliopata nafasi ya kuwepo kwenye maeneo ya tamaduni zingine na ambao wanamaandalizi ya lazima kwa ajili ya kufikiri nje ya nyanja za tamaduni zao. Mtu mwenye akili iliyotayari kupokea desturi zake ni yule anayefaidika. Kuwa na uelewa safi wa utamaduni wa mtu mwingine hutoa uwezekano wa kuchagua.

Maadhimisho ya siku ya tamaduni kwenye nyumba Kuu ya ASC yalikuwa ni jaribio la kusaidia kufahamu utajiri wa tamaduni wa jumuiya ya kimataifa na ule wa majirani, kumpa kila mtu uwezekano wa "kujisikia ndani" na kujibu kwa uaminifu swali hili: "Lini ninajisikia wasiwasi na kitu ambacho sijakizoea?" Kwa maneno mengine, lini ninakuwa tayari kuingia kwenye mang'amuzi mapya ambayo yananilazimu kuacha kitu? Siku ilikuwa imeandaliwa kabla na mwaliko ulikuwa umesambazwa kwenye jumuiya zingine za kimataifa za majirani. Katika makundi kadiri ya mataifa au mtu mmojamoja, kila mmoja alipanga kwa makini na kwa hamu kubwa maonyesho ya baadhi ya vitu vya utamaduni wake, mapishi, nyimbo na mavazi. Baadhi walipanga na wale waliotoka nchi moja walio majirani na hivyo kupanua duara la mahusiano na la washiriki kwenye sherehe. Nyumba ilichangamka wakati ambapo watu walipoanza kuja ili kupata vitu kwa ajili ya kupika, kwa ajili ya kufanya mazoezi ya nyimbo, kwa ajili ya kupamba chumba cha chakula n.k. Uwepo wa waseminari wa Rosminiani kwa danzi na mziki wao uliongeza sana umotomoto na furaha kwenye sherehe. Siku ilikuwa nzuri sana kwa ajili ya roho ya umoja, urafiki na "nafasi mpya" kwa ajili ya uelewano ambao ulikuwa umefunguliwa katika akili zetu na katika mioyo yetu.

Shukrani zetu ziende kwa wale waliopata wazo la kuanzisha jambo hili na wale wote ambao walilipokea na wakachangia kwa ukarimu kulifanya ling'ae.

Kwa kuishi katika mazingira ya mwingiliano wa tamaduni inamaanisha kuwa na udhia kama mwenza katika safari. Ni sehemu ya mchakato wa mabadiliko ambayo tunavuka wakati huo huo

# Nafasi kwa uongozi mkuu



tunnaleta matazamio mapya, tukifikiri upya nia zetu, kuunganisha mawazo yetu ya zamani na mapya na mwisho kuunda mtazamo mpya wa dunia.

Ndio, mabadiliko huanza na hatua ndogo ambazo huacha athari kuelekea mwisho.

**Sr. Bridget Pulickakunnel ASC**



## ENEO LA BARA AFRICA
## Region Tanzania

# HUDUMA KWA MPENDWA JIRANI



Tunatambua kuwa kila mtu ni thamani ya Damu ya Kristo. Kwa maana hiyo Region yetu inatoa huduma mbalimbali. Moja ya huduma hizi ni kuwasaidia watu masikini ili nao waweze kuishi kwa heshima miongoni mwa jamii. Masikini wengi wanapiga hodi katika milango yetu wakiwa na matumaini kuwa watapata msaada kutoka kwetu. Mpaka sasa tumeweza kuwasaidia kadiri ya uwezo wetu kwa kupitia elimu na mahitaji mengine.

Ni miaka takribani saba tangu tumekuwa na watoto wawili wanaokaa nasi. Mmoja anaitwa Sabina, anasoma katika shule ya msingi darasa la tano. Mwingine anaitwa Maria, anasoma katika shule ya msingi darasa la sita. Tunamshukuru Mungu kwani wote wawili wanaendelea vizuri na masomo yao. Kila mmoja wao ana historia yake ya maisha. Sabina alichukuliwa na masista wa jumuiya ya Morogoro kutoka katika familia ya



mjomba wake. Masista walimchukua kwa sababu mke wa mjomba wake alikuwa akimtesa sana.

Sabina alichukuliwa na mjomba wake baada ya mama yake kuolewa na mwanaume mwingine. Mwanaume huyo alikataa kumpokea na kumlea kwa kuwa siyo mtoto wake. Hapo ndipo Sabina alipojikuta akiangukia mikononi mwa mama mkatili aliyempiga na kutendea kwa ukatili.

Mama yake Maria alifariki wakati Maria akiwa na umri mdogo sana. Aliletwa na baba yake kwenye Kituo cha Afya cha Mtakatifu Maria De Mattias Manyoni. Alipokelewa na kulelewa na Sr. Delphina Gnerre. Hawa ni baadhi ya watoto wahitaji ambao tunawasaidia. Tunatambua kuwa wao pia wana haki ya kulelewa vizuri na kupata huduma zote wanazostahili kama watoto wengine. Tunajitahidi kuwalea vizuri ili wajisikie kupendwa na kupokelewa.



Sabina



Maria

Kwa upande wao, daima wamekuwa na shukrani, wakijitahidi kufanya vizuri katika masomo yao na maisha kwa ujumla. Maria anaishi katika jumuiya ya Novisiati kwa sababu anasoma katika shule ya Mt. Gaspari Del Bufalo iliyoko karibu na nyumba ya Novisiati. Sabina anasoma katika shule ya jimbo iliyoko mkoa wa Shinyanga mbali na mkoa wa Dodoma, wakati wa likizo anaishi kwenye jumuiya ya nyumba ya Region, Miyuji.

Tunamshukuru Mungu kwa zawadi ya watoto hawa na watoto wengine ambao tumeweza kuwasaidia ili kuwaandalia maisha yao ya baadaye. Tuna nia ya kuwasaidia ili wao nao hapo baadaye waweze kutoa misaada katika familia zao na jamii yao, waondokane na hali ya umasikini na waweze kuishi maisha mazuri kama wengine.

**Sr. Philipina, Roman ASC**

## ENEO LA BARA AMERIKA
## Region Brazili

# MANG'AMUZI MAZURI PAMOJA NA WANANDOA

Umoja wa "Wanandoa Wakikristo" (ECC) ni harakati ya Kanisa Katoliki kwa ajili ya uinjilishaji wa familia na ujenzi wa Ufalme wa Mungu, huko Brazil na katika mataifa mengine, ambayo yanahamasisha mikutano ya kanisa katika ngazi ya parokia.

Umoja wa Wanandoa, Brazili, ulianzishwa mwaka 1970, huko São Paulo na Padri Alfonso Pastore, katika Parokia ya Mama Yetu wa Rosari; unatoa mafunzo ya kiroho kwa wanandoa ukizingatia maisha ya kawaida, unyenyekevu, furaha na sala.

Una lengo la kuinjilisha familia - Kanisa la nyumbani - na una lengo la kupanua upeo wa familia kutoka kwenye mtazamo wa kiparokia, kwenda kwenye ule wa kiulimwengu zaidi.

Mnamo Aprili 28, kijana Zaira Magalhã, mwanasaikolojia wa Hospitali ya Bibi yetu wa Guadalupe, huko Belem, na mimi, kama Mwabuduo Damu ya Kristo, tulialikwa na baadhi ya wanandoa wa ECC, kuratibu moja ya mikutano yao, katika Parokia ya Mt. George, huko barrio Marambaia nje ya mji wa Belém.

Mada ilikuwa: "Msongo wa mawazo ", kama sababu ya kugawanyika kwa familia. Wanandoa 32 walishiriki ambapo, tulianza kwa michoro yenye maelezo ilizoandaliwa kwa ajili ya tukio hilo, walipendekeza tafakari zao na walijihusisha kikamilifu katika kikundi.

Dondoo kuu za mada zilikuwa ni: dhana ya msongo wa mawazo, tabia ya kimwili na ya kihisia, sababu, dalili na athari kwa mtu binafsi na





kwa familia.

Mwisho wa mkutano, tulisherehekea siku za kuzaliwa kwa furaha kwa vitafunwa vitamu sana.

Paroko alisaidia maandalizi kwa ushiriki wake na kutoa tafakari kwa namna ya kirafiki.

**Sr. Maria José Dutra, ASC**



### ENEO BARA ASIA
### Region Philippine

# MPANGO MZURI SANA WA BARA LA ASIA KWA WAABUDUO WETU WA NADHIRI ZA MUDA HUKO PHILIPPINE

Ni Jumatatu asubuhi, tarehe 23 Aprili 2018. Tunajiandaa kwa somo letu la kwanza kwa njia ya skype pamoja na Waabuduo wawili wa Vietnam tumekaa mezani na Waabuduo wawili wa India wako pamoja nasi kiroho tu. Bila shaka, kwa sababu ya matatizo ya visa, wamejikuta bado wako India, lakini tumejaa matumaini kuwa watafika hivi karibuni!




Sr. Mary Kevin Rooney anatuma ujumbe wa mwisho kwa njia ya Skype kwa Sr. Joan Hornick ambao unasema jambo Fulani: "LEO (bila shaka) tutapokea printa mpya, ASUBUHI HII (bila shaka) watu wa mlango unaofuata wanatumia msumeno mduara. ALFAJIRI (bila shaka) kuna baridi kama "majira ya baridi" na asubuhi mbwa wanabweka pamoja (bila shaka) naona kuwa kiongozi wa kundi anaangalia kwa jicho kali ili kujikinga na kitu chochote ambacho chaweza kudhuru. Nawaambieni itakuwa siku kubwa !!!!!!!!!!!!!! "

Kwa kweli alikuwa Sr. Joan Hornick alianza kipindi cha kwanza kabisa na sisi na mada ilikuwa ile ya MABADILIKO! Mtiririko wa maneno ulikuwa polepole, masikio yetu yalisikiliza kwa makini namna mpya alyokuwa anatamka na yalikuwa tayari kwa Kile TULICHOFAHAMU kuwa kiingekuwa muhimu sana kukua katika uelewa, kiutu na katika hekima inayotoka kwa wote waliowazee na waliopo ambao wapo katika maisha yetu mpaka sasa.

Wanawake hawa wameonja "kwa heri" nyingi katika maisha kama wengi wetu tunavyoweza kufikiri: kwenda Korea kujifunza lugha ili kujibu wito wa ndani kuwa Waabuduo, na sasa kujifunza Kiingereza ili kushiriki katika mpango huu kwa maendeleo na yote yamesababishwa na lugha ile ile ya upendo ambayo inaambatana na karama yetu ya Waabuduo.

Ni zawadi ya kuweza kuambatana nayo katika awamu hii ya safari yao katika maandalizi ya nadhiri za daima. Tunajumuisha picha za matukio yetu ASC. Kutakuwa na mengine mengi! Mtuombee.

**Sr. Mai, Sr.Hien, (pia Sr. Jancy na SR. Roja), Sr. Mary Kevin, Waabuduo wote**

## ENEO LA BARA ULAYA
## Region Italia

# ZIARA YA MWISHO HUKO PHILIPPINE



Miezi sita baada ya kuondoka kwangu toka Mji wa Quezon, kwa maumivu lakini lazima ili kuweza kujibu mwito wa utume mpya niliopewa. Tarehe 26 Mwezi Machi uliopita nilipata nafasi ya kurudi tena kwenye eneo hilo nilipendalo sana. Safari kutoka Italia hadi Manila, licha ya masaa 14 ya ndege, ilionekana fupi na masista walikuwa pale kunipokea kwa furaha. Muda wangu wa kukaa Philippine ulikuwa wa wiki tatu, nilijua kuwa muda ungepita haraka na kwamba kila wakati, ungekuwa ni zawadi ya kuiishi kwa furaha na utayari; kwa kweli nilikuwa natambua kuwa kazi yangu, kujihusisha kwangu na kuwa kwangu chini ya Foundation kungemalizika kwa ziara hii. Nilipofika pale, masista wote walioko Philippine walikuwa wamekusanyika kwenye nyumba kuu kwa maadhimisho ya Juma Kuu na kwa ajili ya mafungo ya kiroho ya mwaka kwa ajili ya maandalizi ya mkutano wa Foundation. Hata Sr. Mary Kevin Rooney alikuwa amefika kutoka Amerika siku chache zilizopita, alikuwa ameungana na kikundi. Yeye atakuwa pale hadi mwezi Disemba. Sr. Mary Kevin pamoja na Sr. Manjusha Joseph, wa India, na ASC vijana wa Vietnam na ASC vijana wa India wataunda jumuiya ya masista wenye nadhiri za muda wa eneo la Bara la Asia.

Wakati wa siku za kukaa huko nimeonja tena mara nyingine, kwa furaha kubwa jinsi Foundation ilivyo ndogo kiuhalisia lakini iliyo hai. Mashirikisho ya masista kwenye Mkutano, chaguzi zilizofanywa katika miaka hii ya mwisho, maamuzi ya kupanua uwepo wa ASC kutoka Kaskazini hadi Katikati ya Philippine, kujihusisha katika utume mpya kwa ajili ya kuwasaidia vijana na kwa ajili ya huduma ya Kanisa mahalia, hayo yote yamenitia nguvu. Uhai unaonekana pia kupitia utayari kwa haya mang'amuzi ya mchanganyiko wa tamaduni na mataifa wa masista vijana wa eneo la Bara, ambalo linapokea utofauti wa ASC kutoka Asia na kutoka Amerika, kwa ajili ya kipindi cha malezi.

Masista wa Foundation wanaonyesha hilo, kupitia chaguzi za kila siku kuambatana na "wadogo" wakisaidia na kuhudumia wasichana wenye shida kwa kuwapa mafunzo ya kutwa kwenye kituo na kwa huduma ya afya kwa masikini na waliotengwa. Katika kazi hii, ni mtindo wao kujishughulisha na kuwafanya watu walio matajiri zaidi kuwa na huruma, ili waweze kushirikisha katika umoja na uwajibikaji mali zao na walio maskini zaidi. Kurudi tena pale kumenifanya kufikiri tena safari iliyofanyika katika miaka hii ambayo imenipa changamoto kukua katika kupokea utofauti, mang'amuzi ambayo si kila mara yalikuwa rahisi. Uhakika ya kwamba maisha mapya yanaweza kuzaa, tu kutokana na mbegu iliyotupwa ardhini ambayo inakubali kufa, daima umenisindikiza katika nyakati za vipingamizi, mashaka, za hatari.

Ninamshukuru sana kila sista mwabuduo wa Foundation kwa kunipa nafasi ya kutembea pamoja, kushirikishana furaha katika mafanikio, bidii katika ndoto na kutiana moyo kutumaini katika nyakati ngumu. Nawashukuru marafiki wote, hasa familia ya Franco, kwa kunifanya daima nijisikie nyumbani, kwa upendo, msaada, uaminifu na heshima. Shukrani kwa wafanyakazi wa Kituo cha Mission "Mt. Maria De Mattias" ambao, kwa imani, wanatembea katika imani ndani ya Kristo na kuamini katika tunu za maisha, kwa kuwa tayari kwa huduma za kujitolea bure kwa walio wahitaji zaidi, kwa wagonjwa ambao, kwa imani, walituwezesha kuwahudumia kwa vipaji vyetu na mapungufu yetu, katika kujaribu kushuhudia kuwa upendo wa Yesu huponya, nguvu ya Damu yake huokoa, na maisha ni zawadi ya thamani ya kuilinda, kuitetea na kuipenda kwa sababu ni zawadi ya Mungu daima.

**Sr. Maria Grazia Boccamazzo, ASC**

## ENEO LA BARA ULAYA
## Region Italia

# MAADHIMISHO YA WATU



Katika kipindi kinachosifika kwa kukutanisha tamaduni tofauti na mara nyingi za kutoka mbali, tumesikia hamu, kama jumuiya ya kimataifa, kutenga siku kwa ajili ya kusherehekea mchanganyiko wa tamaduni. Tarehe 21 mwezi Aprili uliopita, nyumba kuu ilitoa nafasi na muda kwa ajili ya "Maadhimisho ya watu" ambapo walishiriki waseminari mbalimbali wa Warosmini na baadhi ya masista wa jumuiya ya nyumba ya Region, San Giovanni. Kila utamaduni ulichagua chakula kimoja ili kuwakilisha taifa lake. Kwenye nyumba kuu kuna uwepo wa nchi 8 tofauti (Benin, Brazili, Korea, Croazia, India, Italia, Poland na USA) ambazo siku ya sherehe iliongezeka pia Kenya na Tanzania. Kwa siku mbili jiko letu lilikuwa ukumbi wa ubunifu wa vyakula vizuri na vitamu pamoja na kinywaji kitamu kiitwacho caipirinha cha Brazil, vyakula viliwavyo kabla ya mlo na vitafunwa vya USA; ugali mweupe na mchuzi wa samaki na maandazi ya Benin, cevap na pita sa sirom vya Croazia; palappam ya India, vyakula vya kuoka na nyama vya Italia; wali wa nyama wa Korea na keki ya asali ya Poland. Waseminari Warosmini wa Tanzania walileta chakula cha kitanzania kinachoandalia siku ya ndoa, ndizi na nyama ya ng'ombe, wakati wale wa India walileta wali uliondaliwa kwa limau. Chumba chetu cha chakula kilipambwa kwa pendera na vitambaa vya rangi na meza zilizoandaliwa zilikuwa zinaonyesha sherehe ya kweli machoni na kwa "tumbo".

Zaidi ya kuonja utamu wa chakula, kilichotufurahisha zaidi ilikuwa ni kukaa pamoja na kushirikishana sehemu za utajiri wetu wa tamaduni. Kila taifa lilionyesha wimbo au mchezo na hata wafanyakazi wetu walituimbia wimbo wa kirumi.



Daima kukaa pamoja kulirahisisha ujengaji wa mahusiano, mabadilishano ya mawazo, mashirikisho ya ujuzi... Yesu alijua hilo vizuri na hakika alikaa mezani ili kuadhimisha Pasaka, agano jipya na la milele ambalo alilitia muhuri kwa Damu yake.

Katika udogo wetu tulipenda kutoa alama ya uwazi na kupokeana kwa tumaini na hamu ya kukua daima zaidi kama jumuiya yenye tamaduni mbalimbali na ya kimataifa.

**Sr. Barbara Perali**

## ENEO LA BARA ULAYA
## Region Zagreb

# SIKU YA ASC WA REGION YA ZAGABRIA

Namna ya kawaida ya kusherehekea Siku ya ASC wa Region ya Zagabria imekuwa sasa mapokeo ya kusanyiko la kawaida ambalo si tu kati ya waabuduo bali pia kati ya wale wanaofanya kazi pamoja nasi, wanachama wa damu, ASC walioacha shirika, marafiki, maparoko ambao wanashirikiana na ASC, na wale wote ambao wanafuata kwa namna yeyote ile tasaufi ya Damu ya Kristo. Hivyo, mwaka huu tulifanya hija tarehe 14 Aprili huko Karlovac, kwenye Santuari ya Mt. Yoseph, mlinzi wa Mkoa wa Zagabria, na huko Krasic kufuata njia ya Mwenyeheri Alojzije Stepinac.

Kwenye mkutano walishiriki mahujaji 1000 kutoka Croazia, kutoka Bosnia na Erzegovina, kutoka Ausria na Svizzera na ASC 70. Mons. Antun Sente alitupokea na kutubariki kwenye Lango Takatifu la kuingilia la Santuari na Padre Ilija Grgic, CPPS aliongoza adhimisho la Misa pamoja na mapadre nane mahujaji wanaoshirikiana na ASC. Liturjia ilichangamshwa na kwaya ya Mt. Anna wa Bjelovar, iliyoongozwa na Sr. Virginia Kolic pamoja na mwambatano wa kinanda kilichopigwa na Sr. Domagoja Ljubic, ambapo wimbo, ulijaza Amani mioyo na roho. Uliukuwa ni mshikamano wa kihistoria kati ya ASC na mahujaji kutoka: Karlovac, Krasic,  Karlovac na mji ambao kwa miaka 90 umekuwa ukiwapokea ASC. Jumuiya iliyoko Karlovac ilifunguliwa tarehe 13 Januari 1928 na mwishoni mwa mwaka 1945 utume mkuu wa masista ulikuwa utoaji wa chakula kwa masikini na shule ya chekechea. Mwaka 1960 ikifuatia kupewa nyumba moja, masista walifungua karakana na duka moja la vitu vilivyotengenezwa kwa mikono. Toka mwaka 1999 masista wanaishi kwenye nyumba moja mpya. Leo wao wanafanya utume kwenye parokia mbili, wanafundisha katekesi mashuleni, na parokiani, wanaongoza maadhimisho ya liturjia na pamoja na wanachama wa Damu ya Kristo wanafanya kazi kwenye hospitali.

Krasic na vijiji vyake vinavyouzunguka walitoa kwenye Shirika karibu Waabuduo 20. Mwenyeheri Alojzije Stepinac mwenyewe aliwaonesha Shirika la Waabuduo wasichana mbalimbali na baadhi walikuwa ndugu wa Mwenye heri mwenyewe kama Sr. Emanela Jagunic na Sr. Alojzija Zupanac, na mjukuu wake.

**Sr. Danijela Anić, ASC**



# JANA, LEO, KESHO

Wakati nafikiria "muda uliopita" na vyote tulivyo navyo, jumuiya ya afanyakazi wa shule ya watoto "Leptirići" (vipepeo) huko Glamoč, tulikaa na kufikiri juu ya makala ambayo niliombwa kuiandika kuelezea hali ya sasa, nadhani kuwa badala ya makala ningeweza kuandika kitabu. Kwa sababu hii, katika makala hii sikusudii kuongea juu ya muda uliopita, ambao kwa vyovyote vile "umepita", umeshinda. Siwezi kubadili kile tulichoishi kwa sababu wakati uliokwisha pita umefungiwa katika kabati la wakati uliopita... Kile ambacho haiwezekani kukiondoa katika kabati ni "athari za wakati uliopita" kwa sababu bado zipo hapa leo... Leo, sasa.

Siku moja Mungu ameniruhusu kuishi kwa ajili ya utukufu Wake na kwa ajili manufaa ya mpendwa jirani leo. Leo nina nafasi ya kuwashukuru watu wengi wema ambao Mungu amewaweka kwenye njia yangu, ili waweze kunisaidia kubeba msalaba. Leo nataka kutoa shukrani kubwa kwa Padre. Andrej na shirika zima la VIVAT, kwa kukubali kuwa Simon wetu wa Kirene na kuturuhusu tueleze historia yetu na kupeleka umhimu wake kwenye Umoja wa Mataifa, wakionyesha uovu wote ambao sisi, kama jumuiya ya wafanyakazi, tumeuishi kwa miaka.

Kwa bahati mbaya leo hali haijawahi kuboreshwa kulinganisha na iliyopita kwa sababu tunaishi katika Nchi ambayo iinaunda sheria zake na inatoa uwezekano kwa wale wanaowafanyia kazi, wasiweze kulipwa ipasavyo kwa kazi yao. Kwa mujibu wa sheria juu ya taratibu za utekelezaji wa Mahakama ya BH (Bosnia Herzegovina), mtu ambaye hajalipwa na Serikali kwa kazi yake, hata kama atathibitisha mahakamani kuwa ana haki, kwa kweli hawezi kupokea malipo hayo kwa sababu sheria inasema kwamba kiasi ambacho mwanzilishi wa taasisi (kwa upande wetu manispaa) anapaswa kugawa kwa sharti kutoka bajeti yake kwa hukumu zinazowezekana, ni asilimia 0.3 ya bajeti ya makadirio. Fikiria: 0.3% !!!

Kwa upande wetu, manispaa ya Glamoč sasa inadaiwa na wafanyakazi wetu 240,000 KM (zilizobadilishwa katika bidhaa). Kwa mujibu wa sheria, 0.3% ya bajeti, kwa mwaka 2017 tu, ni sawa na 7,300 KM ambazo inapaswa kulipwa. Kwa mujibu wa hukumu ya sasa ya Mahakama mishahara yetu, ile tuliyodai (katika kesi yangu ya mishahara isiyolipwa 55 na kwa wafanyakazi wengine wote 32), italipwa kulingana na kile kilichowekwa na sheria ya sasa katika miaka 30 ijayo. Kwa kawaida, kama sheria ingepaswa ibaki kama ilivyo leo, wakati wetu ujao ungeonekana kuwa wa utukufu zaidi ...Hata hivyo, sitaki kufikiria au kuandika juu ya siku zetu zijazo kama jambo lisilo wazi, kwa sababu najua kuna mtu ambaye atakuwa na neno la mwisho. Yeye anajua kwa nini mimi, kwa nini sasa, na kwa muda gani hali hii itaendelea. Wakati huo huo, mnamo Oktoba 2017, mtu ambaye alikuwa ndiye sababu ya mateso yetu yote, ambaye kama mtu wa kwanza alitenda kwa namna ya ubaguzi kwangu kwa hila zake na matendo yake, na hivyo sasa tunajikuta kukabiliana na uchaguzi mpya.

Tume Kuu ya Uchaguzi imeweka tarehe ya uchaguzi utakaofanyika kwa mshangao na utafanyika huko Glamoč. Orodha za vyama zilitolewa. Ikiwa mgombea wa chama cha SNSD, ambaye sasa ana mamlaka katika Glamoč, atachaguliwa, naamini kwamba hali hiyo inaweza kuboresha kwa sababu mtoto wake anasoma katika shule yetu ya chekechea na anajua matatizo yaliyopo shuleni. Tunatarajia kuwa ataichukulia hali hiyo kwa moyo kwa kuwa mtoto wake anashinda masaa nane kwa siku katika shule yetu ya chekechea. Kwa sababu kile ninachojua juu yake, yeye ni mtu mwenye msimamo katika maamuzi, lakini siasa ni mchezo wa ajabu. Kwa kweli, hakuna kitu kilicho cha uhakika kabisa na siwezi kumsaidia kuwa na hofu kidogo kwani siasa inaweza kumfanya abadili mawazo.

Na katika matumaini ya kile ambacho kitatusaidia kesho... haitabaki tu kuweka kila kitu mikononi mwa Mungu na kuishi katika ukweli. Hata hivyo, matumaini yetu sio kusubiri kesho bila kufanya kitu bali kupokea leo ya kumpenda Yesu katika watoto hawa ambao tumekabidhiwa.

Mwishowe, nitakapokutana na Bwana wa maisha yangu, Bwana wa historia, ambaye ataniuliza ni jinsi gani na kwa kiwango gani nimemtambua yeye katika wale aliowaweka kwenye njia yangu katika maisha, Yeye mwenyewe atanihukumu.

**Sr. Janja Martina Katović, ASC**




# KALENDA YA UONGOZI MKUU

**16-18 Mei** Sherehe ya 15 ya kutangazwa kuwa Mt. Maria De Mattias
**25-31 Mei** Sr Nadia Coppa atatembelea Fooundation ya Hispania
**17-27 Juni** Sr Nadia Coppa na Sr Dani Brought watashiriki Mkutano wa Uchaguzi wa Region ya USA

# SIKU ZA KUZALIWA: *TUNASHEREHEKEA MAISHA*




**Sr. Sivia Guthala**
17.06.1989 India 30° miaka ya
**Sr. Silvery Ngoi Margarita Sita**
06.06.1978 Tanzania 40° miaka ya
**Sr. Domenica Scalera**
19.06.1971 Italia
**Sr Beena Thoombalan**
15.06.1968 India 50° miaka ya
**Sr Luisa Pacifico**
16.06.1948 Italia 70° miaka ya
**Sr Janice Friess**
09.06.1928 USA 90° miaka ya
**Sr. Oliva Trotto**
14.06.1928 Italia 90° miaka ya
**Sr. Giovanna Cinque**
27.06.1928 Italia 90° miaka ya

# WALIORUDI NYUMBANI KWA BABA



20.4. 2018 **Sr Marciana Heimann** USA
24.4.2018 **Sr Rosa Damiani** Italia
8.5.2018 **Sr Mary Anthony Mathews** USA
12.5.2018 **Sr Janis Yaekel** USA

# KUMBUKUMBU ZA NADHIRI

25°
**Sr Anna Grazia Di Liddo**
**Sr Domenica Scalera**

# MIKUTANO YA REGION

21-24 juni
**Mkutano wa Uchaguzi USA**

Gazeti la kimataifa
Waabuduo Damu ya Kristo

... Kwa Neno Lako...

**Taarifa za kila mwezi**

*iliyorekebishwa na*
**Zinazofamjwa na waabuduo damu ya Kristo**
**Mawasiliano ya Kimataifa - Uongozi Mkuu**
via Maria De Mattias, 10 - 00183 ROMA

**Mwaka XX – Namba 8 – Juni 2018**

*Kamati ya ya waandishi wa habarì*
**Maria Grazia Boccamazzo, asc**
**Mimma Scalera, asc**

Inetafsirwa na:
*Kikroasia:* **sr Renata Vukadin**
*Kingeraza :* **sr Betty Adams**
*Kiswahili:* **sr Martina Marco**
*Kipolishi:* **sr Bozena Hulisz - sr Elisbieta Bukis**
*KIreno:* **sr Clara Albuquerque**
*Kispania :* **sr Miriam Ortiz**
*Kijerumani :* **sr Lisbeth Reichlin**